

Maswali

1. Maelfu ya watu walithibitisha namna gani kwamba Yesu ni mwana wa Mungu?
2. Mbona nambari ya wanafunzi viongozi iliongezeka?
3. Mbona makuhani walimlenga Stefano?
4. Walimkamata Stefano kwa mashitaka gani?
5. Jambo kuu liliokuwa na uzito kwa mazungumzo ya Stefano lilikuwa lipi?
6. Stefano aliona nini baada ya kunena?
7. Stefano aliuwawa namna gani?
8. Stefano alisema nini kabla afe?
9. Nani mwingine alisema manano hayo kabla ya kufa?
10. Kifo cha Stefano kilikuwa na matokeo gani kwa waumini wengine?

Majibu

1. Walimuona akiwa hai na mzima kuonyesha amafufuka kutoka kwa wafu.
2. Kwa sababu waumini walikuwa wanaendelea kuongezeka.
3. Kwa sababu alikuwa ameshawishi watu kwamba Yesu ni mwana wa Mungu.
4. Walisema alikuwa amasema mambo yasiyo ya kweli.
5. Stefano aliwaonyesha vile kila mara watu wa Israeli walikuwa wamekataa viongozi waliotumwa na Mungu. Na sasa walikuwa wamekataa Yesu.
6. Aliona Yesu kwa utukufu.
7. Alipigwa mawe.
8. Aliuliza Mungu awasamehe waliokuwa wakimuua.
9. Yesu.
10. Waumini wengi waliondoka Yerusalem kwa sababu waliogopa. Waliendelea kuhubiri juu ya Yesu mahali pengine pengi.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



47 Stefano apigwa mawe

Marejeo

Matendo ya mitume 6 na 7

Kiini cha somo

Stefano alijua kwamba Mungu alikuwa naye. Alihubiri ingawaje alijua watu watamuua.

Maneno maalum

1. Sikitika + Ushahidi
2. Stefano + Usaidizi zaidi + himizo + miujiza
3. Maelfu + nguvu + kasirika
4. Kamata + hekalu + Musa
5. Kutetea + kataliwa kila wakati
6. Utukufu kwa Yesu + samehe
7. Matokeo


47.1 Maelfu ya watu sasa walijua kwamba Yesu alikuwa mwana wa Mungu. Walisikitika kwamba viongozi wao waliomuua walikuwa na ukweli kwamba Yesu alikuwa ako hai na ni mzima, kwa sababu watu wengi wamemuona. Huu ulikuwa ushahidi wa kuonyesha ni mwana wa Mungu.

47.2 Stefano alikuwa na ukweli huu. Alikubaliwa kuungana na kikundi asili cha wanafunzi. Walitaka usaidizi zaidi kwa ajili ya waumuni wengi. Alibatizwa na akawa mfwasi wa kweli wa Yesu. Aligundua kwamba angezungumza hadharani bila uoga. Hata angefanya miujiza.

47.3 Watu wengi sana walibatizwa katika Yesu, wakamwamini na hata kwa Ufalme wa Mungu. Bidii ya Stefano ilifanya utawala umchukie. Maneno yake kuhusu Yesu yalikuwa na nguvu. Hii ilifanya makuhani wakasirike sana. Walifikiri hakutakuwa na mazungumzo juu ya Yesu tena baada ya kumua.

47.4 Walikamata Stefano. Mashitaka yalikuwa eti alizungumza uongo kuhusu Musa na hekalu. Ilikuwa ni hatia kuzungumza vibaya kwa hivi vitu. Stefano hakusema neno lolote la uongo. Alisema yaliyosemwa na Yesu kwamba hekalu itaharibiwa na ijengwe tena. Yesu alizungumza juu ya mwenyewe. Makuhani hawakuelewa.

47.5 Stefano aliletwa kortini. Alikubaliwa kujitetea. Mara tena maneno yake yakawa na nguvu. Waliokuweko wakaona uso wake ulikuwa unametameta. Stefano alizungumzia hadithi ya wayahudi. Alisema katika hadithi yao yote, Mungu aliwalinda kwa sababu alimpenda Ibrahimu. Viongozi wote waliotumwa na Mungu waliwakataa. Kumalizia, alishaambia, "Mko mnakataa Yesu vile mmekataa Mungu kila mara".



47.6 Wakati huo Stefano akaangalia mbinguni. Aliona Yesu kwa utukufu wa mbinguni. Amesimama mkono wa kuume wa Mungu. Lazima ilionekana ya ajabu. Alijaribu kuambia waliokuwa kortini. Walisema alikuwa anakufuru. Walimtoa nje ya korti, na kumpeleka nje wa mji. Walimua kwa kumpiga kwa mawe. Alipokuwa akianguka chini, aliuliza Mungu awasamehe waliokuwa wakimuua. Hata Yesu alisema hivyo wakati alikuwa akifa.

47.7 Mauaji ya Stefano yalikuwa na matokeo mabaya kwa wa waumini. Wengi walihofia usalama wao na wakaogopa kukaa Yerusalem. Waliondoka mjini na kuenda kuishi engine. Walihubiria watu juu ya Yesu popote walipoenda kuishi. Watu wageni walisikia habari ya Yesu.